**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA 2021/2022 ULIOFANYIKA TAREHE 28/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA UALIMU KITANGARI.**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Mhe. Ladda T. Mfaume | - | Diwani Kitangari | - Mwenyekiti |
| 2. Ndg. Duncan G. Thebas | - | Mkurugenzi Mtendaji (W) | -Katibu |
| 3. Mhe. Isabela D. Makumbuli | - | Diwani Maputi | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Kazumari T. Nauma | - | Diwani Chiwonga | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Rashidi H. Lugomba | - | Diwani Nakahako | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Lisinge Y. Abdala | - | Diwani Nandwahi | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Saidi Y. Rahisi | - | Diwani Makukwe | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Chitwanga R. Ndembo | - | Diwani Mtunguru | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Fabian J. Mahanyuka | - | Diwani Mnyambe | - Mjumbe |
| 10. Mhe. Swalehe F. Amri | - | Diwani Chitekete | - Mjumbe |
| 11. Mhe. Joakim M. Mrope | - | Diwani Mkoma II | - Mjumbe |
| 12. Mhe. Zeituni S. Chimula | - | Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 13. Mhe. Selina R. Mwaya | - | Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 14. Mhe. Zakina A. Mduma | - | Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 15. Mhe. Mohamedi Y. Abdala | - | Diwani Mtopwa | - Mjumbe |
| 16. Mhe. Lihanjala S. Saidi | - | Diwani Mnyeu | - Mjumbe |
| 17. Mhe. Habibu B. Chilamula | - | Diwani Nambali | - Mjumbe |
| 18. Mhe. Sharafi S. Nasoro | - | Diwani Mikumbi | - Mjumbe |
| 19. Mhe. Hashimu B. Namawa | - | Diwani M/Mpelepele | - Mjumbe |
| 20. Mhe. Siwanina M. Jazari | - | Diwani Viti Maalum | - Mjumbe |
| 21. Mhe. Akayoha H. Seleman | - | Diwani Mkwedu | - Mjumbe |
| 22. Mhe. Saleh M. Kamtwanje | - | Diwani Mpwapwa | -Mjumbe |
| 23. Mhe. Faiza O. Kahamba | - | Diwani Viti Maalum | -Mjumbe |
| 24. Mhe. Binae S. Amani | - | Diwani Viti Maalum | -Mjumbe |
| 25. Mhe. Asha H. Libanda | - | Diwani Viti Maalum | -Mjumbe |
| 26. Mhe. Ally H. Mwaya | - | Diwani Muungano | - Mjumbe |
| 27. Mhe. Jamal J. Nandonde | - | Diwani Chilangala | - Mjumbe |
| 28. Mhe. Mussa S. Mtuvenge | - | Diwani Chihangu | - Mjumbe |
| 29. Mhe. Hussein S. Hitu | - | Diwani Malatu | - Mjumbe |
| 30. Mhe. Monica L. Mnayahe | - | Diwani Mchemo | - Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

1. Mhe. Maimuna S. Mtanda - Mbunge Newala Vijijini - kwa taarifa

**WAALIKWA**

1. Ndg. Athumani R. Mrope - Katibu wa CCM (W)

2. Ndg. Daniel M. Zenda - Katibu Tawala Wilaya
3. ISP. Edward L. Msilikale - Mkuu wa Polisi Wilaya
4. Ndg. Edward Mukama - Mkuu wa TAKUKURU (W)
5. SSP. Amani M. Mussa - Mkuu wa Gereza (W)
6. Ndg. Alex D. Ndikile - Kaimu Meneja TANECU

**WATAALAMU NA WASHAURI WALIOKUWEPO.**

1. Ndg. Famili T. Mshaghira - Kaimu Afisa Utumishi (W)
2. Ndg. Hamis Mahmoud - Kaimu Afisa Habari
3. Dr. George S. Matiku - Mganga Mkuu (W)
4. Ndg. Sadock Biyogwa - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
5. Ndg. Lucy I. Matem - Afisa Sheria
6. Ndg. Said M. Said - Afisa Utumishi
7. Ndg. Alford Mpanda - Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika (W)
8. Ndg. Magreth Likonda - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
9. Ndg. Innocent Magayane - Mweka Hazina (W)
10. Ndg. Denis Kaguo - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
11. Ndg. Friday Sondasy - Afisa Elimu Sekondari (W)
12. Ndg. Lukumbuso Mbwilo - Afisa Uchaguzi
13. Ndg. Ally M. Said - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
14. Ndg. Sylivester Ngonyani - Kaimu Afisa Mipango (W)
15. Ndg. Tumain Y. Sadick - Kaimu Afisa Usimamizi wa Mazingira (W
16. Ndg. Alphonce M. Kazala - Afisa Ardhi
17. Ndg. Innocent Mahundu - Afisa Ushirika
18. Ndg. Rukia M. Balakali - Afisa Utumishi
19. Ndg. Ponsiana J. Moyo - Afisa Sheria
20. Ndg. Tumaini S. Abdallah - Afisa Biashara
21. Ndg. Dotto Musiba - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
22. Ndg. Mwalusamba E.A - Afisa Ugavi (W)
23. Ndg. Mshamu Y.S - Afisa Tarafa Chilangala
24. Ndg. Nadhim Mkanga - Afisa Tarafa Mkwedu
25. Ndg. Jane F. Mushi - Afisa Tarafa Mchemo
26. Ndg. John P. Hamis - Afisa Tarafa Kitangari
27. Ndg. Bahati S. Mkulia - Mwandishi wa Habari Newala Fm
28. Ndg. Hamisi S. Kundindo - Mwandishi wa Vikao
29. Ndg. Rashid R. Mabaya - Mwandishi wa Vikao

CamScanner

**MUHTASARI NA 01/2021/2022: KUFUNGUA MKUTANO**

Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe, Wageni waalikwa na Wataalam katika Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani robo ya Kwanza 2021/2022 na kuwaomba wajumbe kujadili kwa kina agenda zote zitakazowasilishwa na kuwa wasikivu. Alifungua mkutano saa 06:24 Mchana.

**MUHTASARI NA 02/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO**

Wajumbe walizipitia Agenda na walithibitisha agenda zilizowasilishwa na kuridhia zijadiliwe katika Mkutano.

**MUHTASARI NA 03/2021/2022: KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 07/09/2021.**

Wajumbe waliupitia Muhtasari huo ukurasa hadi ukurasa hakukuwa na marekebisho yeyote, wajumbe waliridhia Muhtasari huo uwekwe saini na kuwa kumbukumbu sahihi ya mkutano.

**MUHTASARI NA. 04/2021/2022: KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA 2021/2022.**

Kaimu Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa hiyo kwa kusema kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo yenye thamani ya Shilingi 9,478,802,002.00/=. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,005,703,263.71/= ni fedha za bakaa za mwaka 2020/2021, na Shilingi 8,388,294,368/=.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Halmashauri imepokea shilingi 312,881,915.00/= Sawa na asilimia 3.30% ambazo ni fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti na Tshs 312,881,915.00/= ni sawa na asilimia 100% ya fedha zote zilizopokelewa.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo.

Mjumbe alihoji kuwa kwa nini fedha za mradi wa WASH bado zipo hadi leo hazijatumika.

Kaimu Afisa Mipango (W) alijibu kuwa maeneo ambayo fedha hizo hazijatumika kulikuwa na changamoto ya maji na mchanga ila kwa sasa fedha hizo zinaendelea kutumika, pia alieleza kuwa changamoto nyingine ni kubadilika kwa mfumo wa malipo kutoka mfumo wa" EPICOR " kuja mfumo wa MUSE ,hivyo matumizi ya fedha hizo yalichelewa kufanyika.

Mjumbe alihoji kuwa fedha zilizopokelewa nje ya bajeti zimepangiwa matumizi gani.

Kaimu Afisa Mipango (W) alijibu kuwa fedha hizo zimeshaanza kutumika maeneo husika.

Mjumbe alihoji kuwa ni shule zipi zilipangiwa matumizi ya hizo fedha.

Kaimu Afisa Mipango (W) alijibu kuwa ni Shule ya Sekondari Mpotola na Makukwe.

## MUHTASARI NA 05/2021/2022 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA KATA ROBO YA KWANZA 2021/2022

### KATA YA KITANGARI

Mhe. Diwani viti maalum Tarafa ya Kitangari aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo katika kata ya Kitangari kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alisema kuwa taarifa hii imejumuisha taarifa za utawala bora, hali ya elimu katika Kata, ustawi wa Wananchi, shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Kata ikiwemo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa ofisi za vijiji, ujenzi wa Ofisi ya Masjara ya Ardhi, Ujenzi wa Ghala la Mazao na ujenzi wa matundu ya vyoo .

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kulikuwa na majadiliano yafuatayo.

Mjumbe alihoji kuwa taarifa inaonyesha Kata ina vijiji vitano na watendaji 6 je usahihi wa taarifa hii ukoje.

Mwenyekiti wa Kamati ya maendeleo ya Kata alijibu kuwa Mtendaji wa sita yuko standi ya Mabasi kitangari hivyo ni sehemu ya mtendaji anafanya kazi katika kata ya Kitangari.

Mjumbe alishauri kuwa warekebishe kwenye Idadi ya walimu baada ya walimu 26 iwekwe walimu 10.

Mjumbe alihoji Kata inampango gani katika kuhamasisha shughuli za kujitolea.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata alijibu kuwa wamejipanga kutoza faini ya shilingi elfu kumi kwa kila Mwananchi ambae hatashiriki shughuli za kujitolea.

Mjumbe alishauri kuwa Waheshimiwa Madiwani wawe wanapitia taarifa zao kabla ya kuziwasilisha Halmashauri.

Mjumbe alihoji kwa nini Watendaji wa Kata hawaalikwi kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani.



CamScanner

Mkurugenzi Mtendaji (W) alijibu kuwa Watendaji wa Kata sio wajumbe aidha kutokana na ufinyu wa bajeti nao unachangia wasialikwe.

## KATA YA MAKUKWE

Mhe. Diwani wa Kata ya Makukwe aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika kata ya Makukwe kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alisema kuwa taarifa hii imejumuisha taarifa za utawala bora, hali ya elimu katika Kata, Ustawi wa wananchi, shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na

utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika kata ikiwemo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, Ujenzi wa Wodi katika Zahanati ya Makukwe na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhika na utekelezaji wake na hakukuwa na majadiliano.

## KATA YA MAKOMA II

Mhe. Diwani wa Kata ya Makoma II aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Kata ya Makoma II kwa kipindi cha robo ya Kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alisema kuwa taarifa hii imejumuisha taarifa za utawala bora, hali ya elimu katika Kata, Ustawi wa Wananchi, shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Kata ikiwemo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa Ofisi za Vijiji, ukarabati wa vyumba vya madarasa,Ujenzi wa nyumba za walimu, ujenzi wa ofisi ya Kata na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhika na utekelezaji wake na hakukuwa na majadiliano.

## KATA YA MTUNGURU

Mhe. Diwani wa Kata ya Mtunguru aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo katika Kata ya Mtunguru kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alisema kuwa taarifa hii imejumuisha taarifa za utawala bora, hali ya elimu katika Kata, Ustawi wa Wananchi, shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Kata ikiwemo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa Ofisi za vijiji, Ujenzi wa Wodi ya wazazi Zahanati ya Mtunguru ,Ujenzi wa nyumba ya Mtumishi Zahanati ya Ngongo, Ujenzi wa Zahanati ya Mango na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhika na utekelezaji wake na hakukuwa na majadiliano.

**KATA YA CHIHANGU**

Mhe. Diwani wa Kata ya Chihangu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo katika Kata ya Chihangu kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo alisema kuwa taarifa hii imejumuisha taarifa za utawala bora, hali

ya elimu katika Kata, ustawi wa Wananchi, shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kata ikiwemo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto Kituo cha Afya Chihangu, na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhika na utekelezaji wake hakukuwa na majadiliano.

**MUHTASARI NA. 06/2021/2022 KUFUNGA MKUTANO**

Mwenyekiti baada ya majadiliano aliwashukuru wajumbe kwa utulivu wao na michango katika mkutano alifunga Mkutano mnamo saa 07:20 mchana.

"U M E T H I B I T I S H W A NA"

KATIBU
JINA: DUNCAN G. T.
SAINI: [signature]

MWENYEKITI.
JINA: LADDA TAMIMU M.
SAINI: [signature]

TAREHE 27/01/2022.